# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1004

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Fasihi ya Kiswahili Elimu ya Sekondari Kidato cha V - VI

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-779-1

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Fasihi ya Kiswahili Elimu ya Sekondari Kidato cha V - VI nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA FASIHI YA KISWAHILI ELIMU YA SEKONDARI
# KIDATO CHA V – VI

# 2023

©Taasisi ya Elimu Tanzania, 2023
Toleo la kwanza, 2023

ISBN: 978-9987-09-779-1

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 35094
14112 Dar es Salaam.

Simu: +255 735 041 168 / 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Muhtasari wa Fasihi ya Kiswahili Elimu ya Sekondari Kidato cha V–VI.* Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu au sehemu yake kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

# Yaliyomo

Orodha ya Majedwali .......... iv
Vifupisho .......... v
Shukurani .......... vi
1.0 Utangulizi .......... 1
2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania .......... 1
3.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha V–VI .......... 2
4.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V – VI .......... 2
5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi .......... 3
6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji .......... 4
6.1 Mwalimu .......... 5
6.2 Mwanafunzi .......... 6
6.3 Mzazi/Mlezi .......... 6
7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji .......... 7
8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji .......... 7
9.0 Upimaji .......... 7
10.0 Idadi ya Vipindi .......... 8
11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji .......... 8
Kidato cha V .......... 9
Kidato cha VI .......... 43
Bibliografia .......... 67

# Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa Kidato cha V–VI ........ 4

Jedwali Na. 2: Mgawanyo wa Alama za Upimaji Endelevu na Tamati ........ 8

Jedwali Na. 3: Maudhui ya Kidato cha V ........ 9

Jedwali Na. 4: Maudhui ya Kidato cha VI ........ 44

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| LAT | Lugha ya Alama Tanzania |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |

# Shukurani

Maandalizi ya Muhtasari wa Fasihi ya Kiswahili Elimu ya Sekondari Kidato cha V–VI yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha uandaaji wa muhtasari huu. Aidha, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wakuza mitaala wa TET. Vilevile, Taasisi inaishukuru kwa dhati Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na mwelekeo utakaowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndilo lengo kuu la Uboreshaji wa Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 Utangulizi

Fasihi ya Kiswahili ni somo la lazima katika ngazi ya Elimu ya Sekondari Kidato cha V–VI kwa mwanafunzi atakayejiunga na tahasusi ambayo Fasihi ya Kiswahili ni somo mojawapo la ujifunzaji. Lengo la kujifunza Fasihi ya Kiswahili ni kukuza maarifa, ujuzi na mwelekeo utakaomwezesha mwanafunzi kumudu misingi na nadharia za fasihi pamoja na kujenga hoja zenye mantiki na ushawishi katika miktadha mbalimbali. Hivyo, mwanafunzi ataweza kukuza utambuzi binafsi, kujiamini, kutathmini na kutafakari kwa kina masuala ya kifasihi na kijamii. Vilevile, mwanafunzi ataweza kuhakiki, kuimba/kughani, kuigiza na kutunga kazi mbalimbali za fasihi ili kukabiliana na mazingira yanayomzunguka katika maisha ya kila siku kwa kujiajiri au kuajiriwa. Aidha, mwanafunzi ataweza kuthamini utamaduni wake na kuelewa tamaduni za jamii nyingine, hivyo kuweza kushirikiana na watu wa kitaifa na kimataifa.

Muhtasari huu umeandaliwa ili kuongoza ufundishaji na ujifunzaji wa Fasihi ya Kiswahili Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI katika Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Muhtasari huu umetafsiri umahiri uliobainishwa kwenye Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI wa Mwaka 2023. Muhtasari unatoa maelekezo yatakayomwezesha mwalimu kuandaa mchakato wa ufundishaji kwa ufanisi. Vilevile, muhtasari unamwezesha mwalimu kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji zitakazokuza uelewa wa Fasihi ya Kiswahili na stadi za karne ya 21 zikiwemo ubunifu, mawasiliano, ushirikiano, fikra tunduizi na utatuzi wa changamoto.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;
(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;
(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;
(d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa, ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya Taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;
(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;
(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na
(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha V–VI

Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha V - VI ni:

(a) Kuimarisha, kupanua na kuendeleza uelewa wa kina wa maarifa, stadi, na mwelekeo alioupata katika Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini;
(b) Kulinda mila na desturi, tunu za taifa, demokrasia, kuthamini haki za binadamu na za kiraia na wajibu na majukumu yanayoendana na haki hizo;
(c) Kukuza tabia ya kujiamini na uwezo wa kujifunza kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia na maarifa ya kinadharia na kiufundi;
(d) Kuimarisha matumizi ya lugha katika mawasiliano ya kitaaluma;
(e) Kuimarisha uwajibikaji katika masuala mtambuka ya kijamii, yakiwemo afya, usalama, usawa wa kijinsia, na utunzaji endelevu wa mazingira;
(f) Kujenga ujuzi na stadi mbalimbali zitakazomwezesha kujiajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake; na
(g) Kumwandaa mwanafunzi kujiunga na vyuo vya elimu ya kati na juu.

## 4.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V – VI

Umahiri wa jumla kwa Sekondari Kidato cha V – VI ni:

(a) Kutumia maarifa na stadi alizozipata katika ngazi ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini kuimarisha na kupanua uelewa wake wa elimu ya jumla;

(b) Kuthamini uraia, tunu za taifa, na haki za binaadamu na za kiraia;
(c) Kujiamini katika ujifunzaji wa nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia na ya kivitendo;
(d) Kutumia stadi za lugha katika kufanya mawasiliano ya kitaaluma.
(e) Kutumia maarifa ya masuala mtambuka kumudu mazingira yanayomzunguka;
(f) Kutumia ujuzi na stadi alizozipata kumwezesha kujiajiri, kuajiriwa na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake;
(g) Kuonesha utayari wa kujiunga na ngazi ya elimu inayofuata.

## 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Umahiri mkuu na umahiri mahususi wa Muhtasari wa Fasihi ya Kiswahili Kidato cha V–VI unabainishwa katika Jedwali Na.1.

**Jedwali Na. 1:** *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa Kidato cha V–VI*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.1 Kumudu dhana na misingi ya fasihi | 1.1.1 Kukuza uelewa wa dhana ya fasihi<br>1.1.2 Kutathmini nadharia za chimbuko la fasihi<br>1.1.3 Kuchambua uhusiano kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi<br>1.1.4 Kuhusianisha fasihi ya Kiswahili na fasihi kwa Kiswahili<br>1.1.5 Kutathmini maendeleo ya fasihi ya Kiswahili kitaifa na kimataifa |
| 1.2 Kuthamini kazi za fasihi | 1.2.1 Kuonesha uelewa wa misingi ya kutathmini kazi za fasihi<br>1.2.2 Kutathmini nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi<br>1.2.3 Kuhakiki kazi za fasihi kwa kutumia misingi na nadharia mbalimbali<br>1.2.4 Kutumia fasihi kutathmini maadili na mitazamo katika jamii |
| 1.3 Kujenga ujumi | 1.3.1 Kumudu mbinu zinazotumika kujenga ujumi katika kazi za fasihi<br>1.3.2 Kutathmini maana mbalimbali za kazi za kifasihi<br>1.3.3 Kutumia fasihi kujenga hoja zenye mantiki na ushawishi |
| 1.4 Kubuni kazi changamani za fasihi | 1.4.1 Kutambua fursa zinazotokana na kazi za fasihi ya Kiswahili<br>1.4.2 Kumudu kanuni za utunzi wa kazi za fasihi<br>1.4.3 Kutunga kazi za kifasihi |

## 6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji hutegemea ushirikiano mzuri baina ya mwalimu, mwanafunzi na mzazi/mlezi. Muhtasari huu unabainisha majukumu ya kila mshiriki ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Fasihi ya Kiswahili.

## 6.1 Mwalimu

Mwalimu anatarajiwa:

(a) Kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kupata umahiri uliokusudiwa katika somo la Fasihi ya Kiswahili;

(b) Kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai na uwezo wa mwanafunzi ili kumwezesha:

   (i) Kujenga umahiri unaohitajika katika Karne ya 21; na

   (ii) Kushiriki kikamilifu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

(c) Kutumia mbinu shirikishi zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji zikiwemo zile zitakazomwezesha mwanafunzi kufikiri, kutafakari na kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali. Mbinu za kufundishia na kujifunzia zinazopendekezwa ni pamoja na kazi za vitendo, utafiti, majadiliano na kazimradi zinazolenga kutatua matatizo halisi katika mazingira ya mwanafunzi. Aidha, mwalimu anahimizwa kutumia njia nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujenzi wa umahiri uliokusudiwa;

(d) Kuandaa darasa salama lenye mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia;

(e) Kutengeneza au kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia;

(f) Kufanya upimaji endelevu mara kwa mara kwa kutumia zana na mbinu za upimaji na tathmini zinazopima nadharia na vitendo zikiwemo bunguabongo, orodhahakiki, majaribio, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi, kazi za vikundi), kazimradi na mkoba wa kazi. Zana na mbinu nyingine ni majaribio kwa vitendo, uwasilishaji, mitihani ya muhula na mtihani wa mwisho;

(g) Kuhakikisha kuwa ujifunzaji na ufundishaji unafanyika kwa haki na usawa kwa kila mwanafunzi bila kujali tofauti zao;

(h) Kumlinda mwanafunzi awapo shuleni;

(i) Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi ya kila siku;

(j) Kubaini mahitaji ya mwanafunzi na kutoa afua stahiki;
(k) Kushirikisha wazazi/walezi na jamii katika hatua mbalimbali za ujifunzaji wa mwanafunzi; na
(l) Kuchopeka masuala mtambuka na TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

## 6.2 Mwanafunzi

Mwanafunzi anatarajiwa:

(a) Kuwa mtendaji mkuu katika mchakato wote wa ujifunzaji;
(b) Kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji ndani na nje ya darasa ili kupata umahiri unaokusudiwa; na
(c) Kushiriki katika kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo vitabu vya kiada, ziada na machapisho mengine kutoka katika maktabamtandao.

## 6.3 Mzazi/mlezi

Mzazi/Mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mtoto katika ujifunzaji;
(b) Kumsimamia mtoto kutekeleza kazi zake za kitaaluma pale inapowezekana;
(c) Kuhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani ni rafiki na salama yanayowezesha ujifunzaji
(d) Kufuatilia mwenendo wa tabia ya mtoto;
(e) Kumpatia mtoto vifaa vyote vinavyohitajika katika ujifunzaji;
(f) Kuhakikisha mtoto anapata mahitaji muhimu; na
(g) Kumfundisha mtoto kuhusu umuhimu na thamani ya elimu pamoja na kumhimiza kujifunza kwa bidii.

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ni msingi katika kujenga umahiri kwa mwanafunzi. Muhtasari huu unapendekeza mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kila shughuli. Miongoni mwa mbinu hizo ni ziara za kimasomo, kazi za vitendo, masimulizi, majadiliano, fikiri-andika-jozisha-shirikisha na kazimradi. Hata hivyo, mwalimu anashauriwa kutumia mbinu nyingine kama hizo kulingana na muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji.

## 8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unahitaji zana mbalimbali ili kujenga umahiri uliokusudiwa. Hivyo, mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kushirikiana katika kuandaa au kufaragua zana mbadala zinazopatikana katika mazingira ya shuleni na nyumbani pindi zinapohitajika. Vilevile, mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kutafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ili kuleta ufanisi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa kutumika kwa ajili ya rejea vitatolewa na TET.

## 9.0 Upimaji

Upimaji ni mchakato muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Fasihi ya Kiswahili. Mwalimu anashauriwa kuwa na uwanja mpana wa uchaguzi wa mbinu na zana za upimaji wa Fasihi ya Kiswahili ili kupima uwezo wa mwanafunzi katika kukuza uelewa wa fasihi kwa jumla, kuhakiki, na kubuni kazi za fasihi simulizi na andishi pamoja na kujenga hoja zenye mantiki na ushawishi katika miktadha mbalimbali. Zana zinazoweza kutumika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji ni bunguabongo, orodhahakiki, mazoezi ya darasani, majaribio, majaribio kwa vitendo, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi za vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi), kazimradi, mkoba wa kazi na zana nyingine kama hizo. Aidha, upimaji wa somo hili utajumuisha upimaji endelevu na tamati. Upimaji endelevu utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji na utamwezesha mwalimu kubaini uwezo na uhitaji wa mwanafunzi katika ujifunzaji. Hivyo, upimaji endelevu utachangia asilimia 30 ya upimaji wote na upimaji tamati utabeba asilimia 70. Mgawanyo wa alama za upimaji endelevu na tamati umebainishwa katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2:** *Mgawanyo wa Alama za Upimaji Endelevu na Tamati*

| Upimaji | Kidato cha V | Kidato cha VI |
|---|---|---|
| Mtihani wa muhula wa kwanza | 5% | 6% |
| Mtihani wa muhula wa pili | 5% | - |
| Kazimradi (kutunga kazi za fasihi) | - | 7% |
| Mtihani wa Utamilifu wa Kidato cha VI | - | 7% |
| Mtihani wa Taifa | - | 70% |
| **Jumla** | **100%** | |

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Fasihi ya Kiswahili Kidato cha V-VI unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ujifunzaji na ufundishaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za ujifunzaji. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi, ambapo kila kipindi ni dakika 40. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni kumi (10) kwa wiki.

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Maudhui ya muhtasari huu yamepangiliwa katika jedwali lenye vipengele saba ambavyo ni umahiri mkuu, umahiri mahususi, vigezo vya upimaji, shughuli za ujifunzaji, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa, zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa na idadi ya vipindi. Maudhui hayo yameoneshwa katika Jedwali Na. 3 na 4.

## Kidato cha V

**Jedwali Na. 3:** *Maudhui ya Kidato cha V*

| **Umahiri mkuu** | **Umahiri mahususi** | **Shughuli za ujifunzaji** | **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | **Vigezo vya upimaji** | **Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu dhana na misingi ya fasihi | 1.1 Kukuza uelewa wa dhana ya fasihi | (a) Kufafanua dhana ya fasihi kwa kurejelea wataalamu mbalimbali | **Bunguabongo:** Waongoze wanafunzi kubungua bongo kuhusu dhana, sifa na umuhimu wa fasihi<br>**Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili dhana ya fasihi kwa mawanda mapana kwa kurejelea fasili za wataalamu mbalimbali, kisha wajadili sifa na umuhimu wa fasihi katika maisha ya kila siku | Dhana ya fasihi kwa kurejelea wataalamu imefafanuliwa | Mchoro wa sanaa na matawi yake, matini za kifasihi, kamusi, chati ya alama za LAT | 15 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kujadili mitazamo mbalimbali kuhusu dhana ya fasihi | **Igizodhima:** Waongoze wanafunzi kuigiza igizo fupi linaloendana na mazingira yao, kisha waeleze mitazamo yao kuhusiana na igizo hilo<br><br>**Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua matini zinazohusu mitazamo mbalimbali ya fasihi, kisha wabainishe mawazo ya wataalamu hao kuhusu fasihi | Mitazamo mbalimbali kuhusu dhana ya fasihi imejadiliwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kujadili ubora na udhaifu kuhusu mitazamo ya dhana ya fasihi | **Ramani ya dhana:** Kwa kutumia ramani ya dhana waongoze wanafunzi kuchunguza na kuibua hoja za ubora na udhaifu wa mitazamo ya dhana ya fasihi<br><br>**Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili kuhusu ubora na udhaifu wa mitazamo ya dhana ya fasihi | Ubora na udhaifu kuhusu mitazamo ya fasihi imejadiliwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.2 Kutathmini nadharia za chimbuko la fasihi | (a) Kujadili nadharia za chimbuko la fasihi | **Masimulizi:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kusimulia hadithi/visa mbalimbali, kisha wajadili asili/ chimbuko la hadithi/ visa hivyo<br><br>**Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua matini mbalimbali za nadharia za chimbuko la fasihi, kisha wawasilishe kwa ajili ya maboresho. | Nadharia za chimbuko la fasihi zimejadiliwa | Chati yenye nadharia za chimbuko la fasihi, matini na makala za kifasihi, maudhui ya nadharia za chimbuko la fasihi yaliyorekodiwa, magazeti, kamusi, chati ya alama za LAT | 10 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili ubora na udhaifu wa nadharia za chimbuko la fasihi | | | |
| | 1.3 Kuchambua uhusiano kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi | (a) Kufafanua tanzu na vipera vya fasihi simulizi na fasihi andishi | **Ramani ya dhana:** Waongoze wanafunzi kubainisha tanzu na vipera vya fasihi simulizi na fasihi andishi kutokana na michoro waliyopewa | Tanzu na vipera vya fasihi simulizi na fasihi andishi zimefafanuliwa | Chati/ mti wenye tanzu za fasihi simulizi na fasihi andishi, nyimbo, mashairi na maigizo yaliyorekodiwa, matini na makala za kifasihi, magazeti, kamusi, chati ya alama za LAT | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Changanya kete:** Waongoze wanafunzi katika vikundi wakiwa na namba kufafanua tanzu na vipera vya fasihi simulizi (kila kikundi kishughulikie utanzu/kipera chake)<br><br>**Matembezi msambao:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili tanzu na vipera vya fasihi andishi, kisha wabandike kazi hizo darasani kwa ajili ya kuzisoma na majadiliano | | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kueleza mchango wa fasihi simulizi katika maendeleo ya fasihi andishi | **Mdahalo:** Waongoze wanafunzi kufanya mdahalo kuhusu umuhimu wa fasihi simulizi katika maendeleo ya fasihi andishi, kisha litolewe hitimisho | Mchango wa fasihi simulizi katika maendeleo ya fasihi andishi umeelezwa | | |
| | | (c) Kutathmini athari za sayansi na teknolojia katika maendeleo ya fasihi simulizi na fasihi andishi | **Ziara:** Waongoze wanafunzi kutembelea sehemu za kurekodia na kuchapishia kazi za fasihi simulizi na fasihi andishi ili wachunguze namna vifaa vya teknolojia vinavyohusika na uandaaji wa kazi za fasihi. | Athari za sayansi na teknolojia katika maendeleo ya fasihi simulizi zimetathminiwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waongoze wanafunzi kufanya majadiliano ya walichojifunza ziarani<br><br>**Kazimradi:** Wape wanafunzi kazi katika vikundi ya kuangalia/ kusikiliza vipindi vyenye kazi za fasihi katika redio, runinga na mitandao ya kijamii pamoja na kusoma magazeti na matini za fasihi, halafu waeleze athari za sayansi na teknolojia katika maendeleo ya fasihi simulizi na fasihi andishi. Wanafunzi waandike ripoti na kuiwasilisha | | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kujadili mchango wa fasihi simulizi na fasihi andishi katika maendeleo ya jamii | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili mchango wa kazi za fasihi simulizi na andishi katika maendeleo ya jamii | Mchango wa fasihi simulizi na andishi katika maendeleo ya jamii umejadiliwa | | |
| | | (e) Kuhusianisha fasihi simulizi na fasihi andishi | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili sifa za fasihi simulizi na fasihi andishi, kisha kutokana na sifa hizo, wahusianishe fasihi simulizi na fasihi andishi. | Fasihi simulizi na fasihi andishi zimehusianishwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kuthamini kazi za fasihi | 2.1 Kuonesha uelewa wa misingi ya kutathmini kazi za fasihi | (a) Kujadili mitazamo inayohusu fani na maudhui | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua matini zinazohusu mitazamo ya fani na maudhui<br><br>**Changanyakete**: Waongoze wanafunzi wakiwa na namba katika vikundi kujadili mitazamo ya fani na maudhui<br><br>**Mdahalo:** Waongoze wanafunzi kufanya mdahalo kuhusu fani na maudhui kwa kubainisha mitazamo yao kuhusu dhana hizo | Mitazamo inayohusu fani na maudhui imejadiliwa | Chati/mti wenye vipengele vya fani na maudhui ya fani yaliyorekodiwa | 15 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuhusianisha fani na maudhui katika kazi za fasihi | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili uhusiano wa fani na maudhui katika kazi za fasihi | Fani na maudhui katika kazi za fasihi zimehusianishwa | | |
| | | (c) Kueleza dhima za vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi | **Maswali na majibu:** Kwa kutumia maswali, waongoze wanafunzi kueleza dhima za vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi | Dhima za vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi zimeelezwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2 Kutathmini nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi | (a) Kuchambua nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi | **Bunguabongo:** Waongoze wanafunzi kubungua bongo kuhusu dhana, sifa na umuhimu wa nadharia<br><br>**Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kusoma matini zinazohusu nadharia za uhakiki wa fasihi kisha wachambue sifa na misingi ya nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi. | Nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi zimechambuliwa | Chati yenye nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi, chati ya alama za LAT, kamusi, matini na makala za kifasihi | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Kumwalika mgeni:** Mwalike mgeni ambaye ni mahiri katika uga wa fasihi ili afafanue kuhusu dhana, waasisi, misingi, na umuhimu wa nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi<br><br>**Tafakuri:** Waongoze wanafunzi kufanya tafakuri kuhusu nadharia walizojifunza kutoka kwa mgeni mwalikwa. | | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili ubora na udhaifu wa nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi | | | |
| | 2.3 Kuhakiki kazi za fasihi kwa kutumia misingi na nadharia mbalimbali | (a) Kutumia nadharia kuhakiki kazi za fasihi simulizi (*maigizo*) na fasihi andishi (*mashairi na tamthiliya*) za waandishi wakongwe na chipukizi walioteuliwa | **Onesho mbinu:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuangalia maigizo mafupi kwa kutumia vifaa vya TEHAMA, kisha wahakiki maigizo hayo kwa kutumia nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi | Kazi za fasihi simulizi (maigizo) na fasihi andishi (mashairi na tamthiliya) za waandishi wakongwe na chipukizi walioteuliwa zimehakikiwa kwa kutumia misingi na | Matini na makala za kifasihi, magazeti, maigizo, mashairi na tamthiliya zilizorekodiwa, kamusi, vitabu teule, chati ya alama za LAT | 58 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Kazi za vitendo:** Waongoze wanafunzi kughani mashairi kisha wahakiki mawazo/ masuala yanayojitokeza katika mashairi hayo<br><br>**Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kutumia nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi kuchambua mashairi teule ya waandishi wakongwe na chipukizi | nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Kazi za vitendo:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua tamthiliya teule za waandishi wakongwe na waandishi chipukizi kwa kutumia nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi, kisha wawasilishe kazi zao kwa ajili ya maboresho. | | | |
| | | (b) Kutathmini mchango wa nadharia za uhakiki katika maendeleo ya ushairi na tamthiliya | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili mchango wa nadharia za uhakiki wa fasihi katika maendeleo ya ushairi na tamthiliya | Mchango wa nadharia za uhakiki katika maendeleo ya ushairi na tamthiliya zimetathminiwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.4 Kutumia fasihi kutathmini maadili na mitazamo katika jamii | (a) Kueleza maadili yaliyomo katika nyimbo za bongo fleva, mashairi na tamthiliya | **Nyimbo:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kusikiliza nyimbo za bongo fleva za vipindi mbalimbali, kisha wachambue maadili yaliyomo katika nyimbo hizo<br><br>**Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua maadili yaliyomo katika bongo fleva na mashairi teule<br><br>**Kazi za vitendo:** Waongoze wanafunzi kila mmoja achambue maadili yaliyomo katika tamthiliya teule, kisha wawasilishe kwa ajili ya majadiliano | Maadili yanayotokana na nyimbo za bongo fleva, mashairi na tamthiliya yameelezwa | Matini na makala za kifasihi, magazeti, nyimbo za bongo fleva, mashairi na tamthiliya zilizorekodiwa, vitabu teule, chati ya alama za LAT | 40 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kulinganisha maadili yaliyomo katika bongo fleva, mashairi, tamthiliya na imani za jamii | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuhusianisha maadili yaliyomo katika bongofleva na imani za jamii<br>**Maswali na majibu:** Kwa kutumia maswali na majibu, waongoze wanafunzi kuhusianisha maadili yaliyomo katika mashairi teule na imani za jamii<br>**Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kuhusianisha maadili yaliyomo katika tamthiliya teule na imani za jamii | Maadili yaliyomo katika bongo fleva, mashairi na tamthiliya yamelinganishwa na imani za jamii | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kueleza mitazamo iliyomo katika bongo fleva, mashairi na tamthiliya | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kueleza mitazamo iliyomo katika bongo fleva<br><br>**Mdahalo:** Waongoze wanafunzi kufanya mdahalo ili kueleza mitazamo iliyomo katika mashairi teule, kisha ongoza majadiliano ya pamoja ili kuhitimisha<br><br>**Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kueleza mitazamo iliyomo katika tamthiliya teule | Mitazamo iliyomo katika nyimbo za bongo fleva, mashairi na tamthiliya imeelezwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kuhusianisha mitazamo iliyomo katika nyimbo za bongo fleva, mashairi na tamthiliya na matendo ya jamii | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuhusianisha mitazamo iliyomo katika bongo fleva, mashairi pamoja na tamthiliya na matendo ya jamii | Mitazamo iliyomo katika bongo fleva, mashairi na tamthiliya imehusianishwa na matendo ya jamii | | |
| | | (e) Kujadili namna athari za kiimani na kimitazamo katika bongo fleva, mashairi na tamthiliya zinavyojidhihirisha katika jamii | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili namna athari za kiimani na kimitazamo iliyomo katika nyimbo za bongo fleva, mashairi na tamthiliya zinavyojidhihirisha katika jamii | Namna athari za kiimani na mitazamo iliyomo katika bongo fleva, mashairi na tamthiliya zinavyojidhihirisha katika jamii zimejadiliwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.0 Kujenga ujumi | 3.1 Kumudu mbinu zinazotumika kujenga ujumi katika kazi za fasihi | (a) Kueleza mbinu zinazotumika kujenga ujumi katika kazi za fasihi | **Bunguabongo:** Waongoze wanafunzi kubungua bongo kuhusu maana na vipengele vya ujumi<br><br>**Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua matini za kifasihi, kisha waeleze vipengele vilivyotumika kujenga ujumi katika matini hizo | Mbinu zinazotumika kujenga ujumi katika kazi za fasihi zimeelezwa | Matini na makala za kifasihi, magazeti, hadithi, nyimbo, mashairi na maigizo yaliyorekodiwa, vitabu teule, kamusi | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuchambua mbinu zilizotumika kujenga ujumi katika kazi teule za majigambo, mashairi na tamthiliya | **Onesho mbinu:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuangalia majigambo yanayohusu masuala yaliyomo katika jamii zao kwa kutumia vifaa vya TEHAMA, kisha wachambue vipengele vya ujumi vilivyotumika katika majigambo hayo.<br>**Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua vipengele vya ujumi vilivyotumika katika majigambo na mashairi | Mbinu zilizotumika kujenga ujumi katika majigambo, mashairi na tamthiliya zimechambuliwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Matembezi msambao:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua vipengele vinavyotumika kujenga ujumi katika tamthiliya teule, kisha wawasilishe kazi zao kwa ajili ya majadiliano | | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 3.2 Kutathmini maana mbalimbali za kazi za fasihi | (a) Kuibua maana mbalimbali zinazopatikana katika matini/ insha za kifasihi, mashairi na tamthiliya | **Uchunguzi:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchunguza matini/insha za kifasihi, kisha wafafanue maana na sifa za insha za kifasihi kutokana na matini hizo<br><br>**Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kuchambua maana zinazopatikana katika mashairi na tamthiliya | Maana zinazopatikana katika matini/ insha za kifasihi, mashairi na tamthiliya zimeibuliwa | Matini na makala za kifasihi, magazeti, hadithi, nyimbo, mashairi na maigizo yaliyorekodiwa, vitabu teule, kamusi | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
